MSHINDI MKUU NA MWENYE NGUVU

Habari za asubuhi kwenu. "Pasaka njema" sana kwa kila mmoja wenu! Hii ni moja ya siku kuu kuliko zote, katika ukumbusho wa kufufuka kwa Bwana wetu. Ni moja ya siku kuu kuliko zote katika historia yote ya ulimwengu. Ni ule ufufuo. Nasi tuna furaha sana kuwa hapa, asubuhi ya leo, kwenye siku hii kuu. Na kuona jua likichomoza, na maua yakichipuka duniani, kila kitu kinanena juu ya Pasaka.

Na sasa hebu na tuinamishe vichwa vyetu kwa dakika moja tu.

2 Baba Mungu, tunakuja katika Uwepo Wako. Nasi tunakutarajia Wewe utupe, asubuhi ya leo, baraka kidogo tu ya ziada kutoka Mbinguni, mguso mdogo wa Pasaka nafsini mwetu wenyewe; kwamba, tukitoka hapa, tuweze kusema, kama wale waliotoka Emau, "Je, mioyo yetu haikuwaka ndani yetu, kwa sababu ya Uwepo Wake?" Kwa kuwa, tunaomba katika Jina Lake, na kwa ajili ya utukufu Wake. Amina.

3 Kwenye kitabu cha mwisho, mlango wa 28 wa Injili ya Mathayo Mtakatifu, na kifungu cha 7, ninataka kusoma kwa ajili ya fungu la maneno, tunapoingia kwenye ibada hii.

> *Nanyi nendeni upesi, mkawaambie wanafunzi wake kwamba amefufuka kutoka kwa wafu; tazama, anawatangulia kwenda Galilaya; ndiko mtakakomwona: tazama: haya, nimekwisha waambia.*

4 Kumekuwa na maagizo mengi makuu yaliyopewa mwanadamu na watu wa dunia hii. Lakini kamwe hakujakuwapo na agizo muhimu lililotolewa kama hili, "Nendeni mkawaambie wanafunzi Wake kwamba amefufuka kutoka kwa wafu." Hilo ni agizo kuu. Na njia pekee hili lingeweza kutolewa, ilikuwa ni kwa sababu ilibidi kuwe na ushindi mkuu, kwanza.

5 Kumekuwako na watu katika siku zetu, na katika siku zilizopita, na katika historia kuu ya ulimwengu huu, katika nyanja zake kuu, pana za vita; kumekuwako na washindi wengi wakuu, mambo mengi makuu ambayo yamefanywa kwa ajili ya jamii ya wanadamu.

6 Kwa mfano, ninawazia, wakati nikishuka asubuhi ya leo, nikiamka mapema, wala sikupata nafasi ya kusoma sana. Kwa sababu, kamwe sikujua ni sehemu gani, jana usiku, tungekuwa nayo leo, kati ya mimi na mchungaji, kwenye

ibada. Lakini nikishuka kuja huku, ilitokea niliwazia nini, asubuhi ya leo, lingekuwa bora sana nijualo kuwaambia watu Wake, kuchukua ujumbe. Niliwazia hili, "Nendeni mkawaambie wanafunzi Wake." Sasa, *wanafunzi* Wake ni "wafuasi" Wake. *Mwanafunzi* ni "mtu ambaye anafuata." Nami nikawazia somo hili, la, *Mshindi Mkuu Na Mwenye Nguvu*.

7 Na nikiwazia ni washindi wangapi wakuu tumekuwa nao katika ulimwengu huu, na ni mambo gani makuu wamefanya ili kuyaendeleza na kuyaboresha maisha ya mwanadamu. Nilikuwa nikiwazia juu ya Napoleon mashuhuri, huko nyuma katika siku zake, jinsi ambavyo hakuwa Mfaransa hasa, lakini alikuwa na jambo fulani niani mwake. Kwanza, a—aliidharau Ufaransa, hakuipenda. Alitoka visiwani. Lakini alikuwa na wazo niani mwake, ya kwamba, siku moja kwamba angeshinda. Na sababu ya kuwa na haya niani mwake, ilibidi awe na jambo la kufanyia kazi.

8 Kwa kila mtu, kabla ya kuweza kufanya kazi, huna budi kuwa na kusudi fulani, kibadala fulani, kitu ambacho unafanyia kazi, kwa kusudi la kufanya kazi, kitu cha kufanyia kazi.

9 Na kama sote tujuavyo, kwa kuichukua historia ya Hitler. . . au, si ya Hitler, bali ya—ya Napoleon, kwamba aliutegemea mwezi, na mabadiliko ya nyota. Alifanya kazi hivyo, na akitarajia; kwa sababu kwamba wakati mmoja alifanya hivyo, naye akapata ushindi. Ndipo akaingia Ufaransa, naye akawa shujaa mkuu. Aliwaua watu wengi, kwa sababu wasingekubaliana naye. Naye akaifagia nchi yake yote, akaondoa chochote kilichompinga. Aliifagilia tu kabisa, kwa sababu ilibidi mambo yawe hivyo kwake. Kama asingalifanya hivyo, kungekuwa na kitu kinachompinga wakati wote, na mpango wake mkuu aliokuwa nao niani mwake. Maisha yake mwenyewe yangekuwa hatarini, kwa hiyo ilibidi ufalme wake wote uwe mkamilifu kadiri alivyoweza kuufanya.

10 Ninawazia sasa kwa kuwa mnanifuata katika hili, juu ya Mshindi mkuu ninayemwazia. Kila kitu katika Ufalme Wake hakina budi kimfuate. Hakina budi kuwa moyo, nafsi, na mwili, kwa ajili Yake. Hakuwezi kuwa na chochote kinachompinga. Chochote kilichompinga, ingembidi kukiondolea mbali. Hana budi kuwa na kila kitu upande Wake kabisa. Na wakati . . .

11 Napoleon, alichukua silaha, mizinga, bunduki, magoboli, panga. Naye akatoka na wazo hili moja, ya kwamba angeushinda ulimwengu. Na kwa kweli alifanya hivyo, kwenye umri wa miaka thelathini na mitatu. Alipokuwa kijana, alikuwa ni mkataza pombe. Na umaarufu wake mkuu ulimfanya kuwa na sifa kubwa; nayo ikaingia kwenye mishipa yake, mpaka akafa kwenye umri wa miaka thelathini na mitatu, mlevi sugu. Umaarufu wake, asingeweza kustahimili. Nami namwazia mtu, ambaye katika huu, kwenye umri wa miaka thelathini na mitatu, aliushinda

ulimwengu kisha akafa mlevi sugu, kwa sababu ya sifa yake, na kupoteza kanuni yenyewe aliyokuwa akipigania. Alikuwa—alikuwa aina ya mfano, ama, si mfano, ningesema, bali alikuwa ni chombo cha ibilisi. Na kujaribu kuushinda ulimwengu, naye akashindwa, kwenye umri wa miaka thelathini na mitatu.

12 Lakini, loo, Shujaa huyu mkuu, mwenye nguvu, ninayemzungumzia, kwenye umri wa miaka thelathini na mitatu, alishinda kila kitu kilichokuwa duniani na katika—katika kuzimu. Kwenye umri wa miaka thelathini na mitatu, Mshindi mkuu na mwenye nguvu!

13 Ninawazia juu vita vikuu ambavyo vimepiganwa uwanjani. Tunajua, kumalizana na Napoleon, kwamba alifika mwisho wake kule Waterloo. Nilipata fursa, si muda mrefu uliopita, kutazama mifano iliyotengenezwa ya magofu ya magari yake ya vita, na ya wapanda farasi wa huyo mtu, jinsi walivyolala katika uwanja wa vita. Na magari yaliyolundikana, magurudumu yamevunjika, moja kwa moja uwandani, ambako onyesho hili kuu limefanyiwa.

14 Na ni tofauti jinsi gani: kumwona mtu huyo kwenye umri wa miaka thelathini na mitatu, na fedheha iliyo kule katika kumbukumbu za vita vyake vikubwa na kushinda; na kisha kwenda Yerusalemu, na kutazama kaburi tupu, kama kumbukumbu la Mshindi mkuu na mwenye nguvu.

15 Kwa namna fulani, kuna kitu fulani katika ushindi. Kama tuna kitu tunachopigania, endapo kuna ugonjwa katika mwili wetu, nasi tunapigana kati ya mauti na uzima, ni ushindi wa jinsi gani tunapoona ushindi umepatikana. Kama tunapigana juu ya tabia fulani kuu, au jambo fulani kuu linalotuzonga, wakati hatimaye bendera kuu zinapeperushwa na tumeishinda; ni hisia ya jinsi gani inayotupa, ndani yetu, kwa kuwa basi tunaweza kuwa mshindi.

16 Sasa ninawazia juu ya vita vya mwisho, na jinsi ambavyo wakati Hitler alipokuwa ameiteka Warsaw. Nao Wajerumani walidhani kwamba huo ulikuwa ushindi mkubwa zaidi ambao ungeweza kuwapo, kwa sababu kapteni wao mkuu, Adolf Hitler, mara moja alikuwa amezamisha kila kitu huko Warsaw, akabomoa madaraja, nalo lile daraja kuu likaanguka. Magazeti yalionyesha picha kubwa za kuanguka kwa hilo daraja. Wajerumani wakatembea mtaani, na kupiga ngoma na kupiga filimbi, ndipo maelfu ya ndege zikapita karibu naye, alipopata ushindi wake mkuu wa kwanza. Akitoka kwenda kama Alexander Mkuu, au Napoleon, kuushinda ulimwengu, lakini aliishia wapi? Katika aibu. Bila shaka, aliishia hivyo.

17 Ninaweza kukumbuka walipojenga ile Njia kuu ya Burma. Hapana shaka kuwa . . . kama waliuvuka huo mlima. Baadhi ya hao wavulana wameketi hapa asubuhi ya leo, labda, waliopitia njia hii kuu. Ilikuwa ni kazi ngumu jinsi gani! Ni kazi halisi ya

jinsi gani iliyokuwako, nao walifanya kazi kubwa kiasi gani! Na iligharimu pesa ngapi kujenga hiyo Njia ya Burma, mamilioni ya dola! Wavulana waliopoteza maisha yao, katika kufanya hivyo! Lakini hatimaye, na baada ya kitambo kidogo, wakati maili ya mwisho ya njia ilipokuwa imepitiwa, na wakati njia hiyo ilipokamilika, jinsi sauti za ushindi zilivyotolewa na hao watu! Walikuwa na njia ambayo wangeweza kuivuka hiyo milima nayo, wapate ushindi.

18 Ninawazia juu ya njia nyingine, ambayo siku moja iligharimu maisha ya Bwana wetu mbarikiwa. Haikuwa tu ni barabara hapa duniani, bali ilikuwa ni njia kuu inayoitwa "njia kuu ya utakatifu," ambayo wasio safi hawataipitia, ila wale tu waliotiwa chapa. Ni wale tu walio upande aliopo Yeye, ndio watakaopitia kwenye barabara hii kuu.

19 Ushindi mwingi mkuu umepatikana. Wengi wetu leo tunaweza kukumbuka vizuri juu ya Vita vya Kwanza vya Dunia. Nakumbuka nilipokuwa mvulana mdogo tu, naweza kusikia filimbi zikipigwa; na hata wakulima, mashambani, walisimamisha farasi wao, na kupeperusha kofia zao. Walipiga mayowe. Walipiga makelele. Nini kilikuwa kimetokea? Vita vilikuwa vimekwisha. Ushindi ulipatikana. Ule uchumi mkuu tuliokuwa tukiupigania, hatimaye tulikuwa tumepata ushindi.

20 Ninawazia juu ya vita hivi vya mwisho vya dunia. Niliishi upande mwingine tu wa barabara. Basi wakati filimbi zinapoanza kupigwa, watu walikimbilia viwanjani; wanawake wakiwa wamevaa aproni zao, wakizivua, na kuzipeperusha hewani. Risasi zilivuma mitini. Filimbi zililia. Magari yalikimbia mitaani. Watu wakapiga magoti, na kuinua mikono yao juu. Wakapiga mayowe. Wakalia. Kwa nini? Kwa sababu vita vilikuwa vimekwisha. Na wale waliobarikiwa, hao wavulana wapendwa waliokuwa ng'ambo ya bahari, hivi karibuni wangekuwa wanasafiri kwa meli kurudi nyumbani kwao. Ni ushindi ulioje! Ni wakati wa jinsi gani, na msisimko kwa moyo wowote! Ni yubile iliyoje! Usiku huo, kila mtu alikuwa katika hali nzuri sana, ungeweza kuingia kwenye mgahawa ukala, ukatoka nje pasipo kukilipia, ingekuwa ni sawa. Ungeweza kutumia gari la mtu huyo mwingine, ingekuwa ni sawa. Ungeweza kuomba ulichotaka, na pengine ungekipata. Kwa sababu gani? Ushindi ulipatikana. Hao wavulana walikuwa wanakuja nyumbani. Vyote vilikuwa vimekwisha.

21 Nami ninawazia, ndugu yangu, ni vibaya sana kwamba hisia za namna hiyo haziwezi kudumu wakati wote. Lakini, kwa Mkristo, asubuhi ya leo, ushindi umepatikana. Kengele za furaha zinalia. Vita vimekwisha, kati ya Mungu na mwanadamu. Ushindi umepatikana.

22 Kabla ya ushindi wowote kupatikana, lazima kuwe na gharama kubwa za kulipwa. Loo, gharama zipi! Na wakati

mwingine zina kina sana, na zinasababisha makovu makubwa, kurarua. Lakini, ili tuwe na mlima, hatuna budi kuwa na bonde. Kabla hatujaweza kuwa na mwanga wa jua, hatuna budi kupata mvua. Kabla hatujaweza kuwa na nuru, hatuna budi kupata usiku. Kabla hatujaweza kuwa na ukweli, iliwabidi wawe na makosa, la sivyo usingejua kosa lilikuwa ni kitu gani.

23 Lakini ili kushinda na kupata ushindi wa vita vikuu sana vilivyopata kushindwa, Mtu mmoja alitoka Utukufuni, miaka mingi iliyopita. Wala hakujitwika Mwenyewe mfano wa Malaika. Hakuja kama mtu mashuhuri. Lakini Yeye alikuwa athibitishe ya kwamba haihitaji magoboli na risasi, na mabomu ya atomiki, kushinda vita. Yeye alijivika unyenyekevu, kama mtoto mchanga, na akazaliwa horini. Hata hapakuwapo na mahali pa kuzaliwa Kwake, alipokuja. Nataka muangalie zana mbalimbali za vita, zile alizotumia Yeye.

24 Sasa, jamii ya Adamu yote ilikuwa katika utumwa. Hao hapo, bila tumaini, bila Mungu, bila nafasi, bila rehema, bila chochote ambacho kingeweza kuwasaidia. Adui wakuu, wa maeneo ya chini ya waliopotea, waliwafungia gizani. Hapakuwapo na njia ya kutokea. Hapakuwapo na mtu ambaye angeweza kuwasaidia. Hakuna kitu kingeweza kufanywa. Ilionekana kama hasara tupu, kabisa.

25 Lakini Shujaa wetu, Yule aliyeshuka kutoka kwenye malango ya Utukufu, akijidhili chini!

26 Kwa maana, hapakuwapo na mtu duniani angaliweza kuifanya hiyo kazi. Wote walikuwa, tukinena kilimwengu, kwenye mashua ile ile. Tulikuwa, sote, "tumezaliwa katika dhambi, tukaumbika katika uovu, tukaja ulimwenguni tukisema uongo." Wala hakuna mmoja wetu angeweza kumsaidia mwingine. Tulisimama hatujiwezi, tumeshindwa, machafuko kila upande, sote tumetengana. Hatungeweza kushika sheria na sherehe, kutafuta udhaifu wake na kadhalika, tusingeweza kuzishika. Na ilionekana kama jamii yote ya mwanadamu ilikuwa imeangamia.

27 Ndipo akaja, akashuka. Kwa sababu, "Alikuwako hapo mwanzo," Biblia ilisema, "Yeye alikuwa Neno." Alikuwa ni Logos iliyotoka kwa Mungu. Naye Logos, hapo mwanzo, alikuwa Neno. Naye akafanyika Neno. Ndipo alipopaa juu siku ile tukufu ya Pasaka, Yeye akawa si Neno tu, bali akawa Kuhani Mkuu wa Neno Lake Mwenyewe. Loo, ni jambo tukufu jinsi gani, Ndugu Neville! Hebu fikiria! Yeye si Neno tu, bali Yeye ni Kuhani Mkuu wa Neno Lake Mwenyewe. Tungewezaje kulititilia shaka? Tungewezaje kwenda Kwake na tusiamini kwamba tunapokea kile tunachoomba? Kwa maana, Yeye ni Neno na Mwombezi wa Neno! Logos akawa Neno, naye Neno akafanyika mwili; nao mwili ule ule uliokuwa Neno, ukapokelewa juu Utukufuni,

na sasa ni Kuhani Mkuu akifanya maombezi, Mwenyewe, kwa Neno Lake.

28 Hiyo ndiyo inayohitajika! Hiyo ndiyo nyenzo ambayo Kanisa linayo. Ni silaha ya jinsi gani! Hapajapata kuwa na moja kama Hiyo. Yeye alikuwa Neno. Naye alipokuja, alizaliwa horini. Alikuja kutumia silaha ya u-p-e-n-d-o, upendo, kuushinda ulimwengu; si kwa risasi za jeshi, si kwa bombom na vifaru. Lakini Yeye alikuja kwa namna tofauti. Alikuja kwa namna ya upendo. Alikuwa upendo wa Mungu.

29 Wakati mmoja, nikiwa mvulana mdogo, nilikuwa nikifikiri kwamba Kristo alinipenda, naye Mungu alinichukia; kwa sababu kwamba Kristo alikufa kwa ajili yangu, lakini Mungu alikuwa na kitu dhidi yangu. Lakini nikaja kugundua ya kwamba Kristo ndiye moyo wenyewe wa Mungu. "Mungu aliupenda sana ulimwengu, hata akamtoa Mwanawe pekee, ili kila mtu amwaminiye asipotee, bali awe na Uzima wa Milele."

30 Sasa Yeye alikuja, kwanza, kushinda. Nacho kitu ambacho ibilisi alikuwa ameweka duniani ni chuki. Naye alikuja kushinda chuki. Tunaposhinda vita vyetu, na kadhalika, katika vita vya ulimwengu, daima huacha, sikuzote, chuki; kwa sababu, vita vya namna hiyo ni vya adui. Lakini Kristo alikuja na upendo, kushinda chuki, kuwapenda wale ambao walikuwa hawapendeki. Alikuja na silaha tofauti. Naye akajinyenyekeza Mwenyewe, "akafanywa mdogo punde kuliko Malaika," apate kuonja mauti, na kutoa mfano. Na alipokuwa hapa duniani, alitembea miongoni mwa wanadamu.

31 Alithibitisha silaha Zake za vita, wakati alipowaponya wagonjwa. Alipotwaa biskuti tano na vipande viwili vya samaki, na kuwalisha watu elfu tano, alithibitisha ya kwamba Yeye alikuwa na nguvu juu ya kila atomiki iliyokuwako. Sio kwamba tu alikuza samaki, bali alikuza samaki waliokuwa wamepikwa. Sio kwamba tu alikuza ngano katika biskuti hizo, bali alikuza ngano iliyokuwa imepikwa katika biskuti hizo. Ilionyesha kwamba Yeye alikuwa Mshindi yule mkuu na mwenye nguvu! Si kwamba tu alichota maji kutoka kisimani, bali aliyafanya maji hayo, divai, kutoka kisimani. Alithibitisha alikuwa na Nguvu za kushinda. Naye alipenda, nayo silaha Yake ilikuwa ni upendo. Sasa angalieni.

32 Ndipo alipofanya hivyo, aliposimama siku moja kando ya kaburi la Lazaro, na palikuwa na mtu, aliyekufa, na amezikwa siku nne. Hata wale waliokuwa karibu na hapo, walisema, "Hata sasa ananuka." Pua yake ilikuwa imebonyea, mabuu ya ngozi yametambaa ndani yake. Ndipo Yesu akasimama pale, kama Mshindi mkuu, alipowaambia Martha na Mariamu, aliposimama pale, "Je, sikuwaambia, 'Ikiwa tu mngeamini, mngeuona utukufu wa Mungu'?" Alikuwa amemaliza tu kusema (waliposema, "ndugu yetu amekufa," na kadhalika), Yeye

akasema, "Mimi ndimi ufufuo na Uzima! Yeye aniaminiye Mimi, ajapokufa, atakuwa anaishi. Na kila aishiye na kuniamini Mimi, hatakufa kamwe. Je, sikuwaambia hivi punde kwamba Nguvu hizo za Milele zilizobarikiwa ziko ndani Yangu?" Hakutoa tamshi tu, Yeye aliweza kutekeleza kila kitu alichosema, kwa maana Yeye alikuwa ndiye Mshindi mwenye nguvu.

33 Akiishi ndani Yake, akijizuia, ametiwa utaji kwa mwili wa mwanadamu, kama mwanadamu, bali mle ndani mliishi si mwingine ila Mwenyezi Mungu, aliye mkuu na Mwenye nguvu. Yeye angeweza kuumba upya. Angeweza kuumba vitu vipya. Angeweza kunena, na kile alichoomba kingetolewa katika sekunde hiyo. Lakini, alijinyenyekeza, alijidhili. Alitaka kutoa mfano. Alitaka kuwa Mshindi afaaye, Naye alikuwa hivyo. Sasa, Yeye alijithibitisha Mwenyewe kuwa hivyo.

34 Kama vile nimesema mara nyingi katika mikutano yangu, labda ingetoa ushuhuda asubuhi ya leo, katika kundi hili la watu, katika asubuhi hii nzuri ya Pasaka. Mama mmoja, mfuasi wa kanisa fulani ambalo haliamini katika kuikubali Damu ya Bwana Yesu. "Pasipo kumwaga Damu, hakuna ondoleo la dhambi." Aliniambia ya kwamba huyo Mtu alikuwa ni nabii tu, Mtu mzuri sana, nami nikamfanya Yeye Mungu. Nikasema, "Alikuwa ni Mungu. Alikuwa Mungu."

Akasema, "Unajaribu kumfanya kuwa mkuu kupita kiasi."

35 Nikasema, "Hakuna maneno yanayoweza kuelezea ukuu Wake!" Lugha ya mwanadamu haijawahi kupata usemi huo!

36 Nikizungumza na mtu hivi majuzi, mwanadiplomasia kutoka Washington, DC, naye akasema, kwenye ushuhuda mdogo katika ki—kifungua kinywa ambapo tulihusishwa pamoja, akasema, "Ndugu Branham, nimekuwa Mlutheri maisha yangu yote. Lakini," akasema, "hivi majuzi tukihudhuria uamsho wa mtindo wa kale," kasema, "nilipiga magoti madhabahuni, nami nilitaka kupata tukio na Mungu." Akasema, "Ndipo nilipokuwa pale magotini mwangu. . . " Sasa, huyu ni mwanadiplomasia wa Washington ambaye hata alitumika chini ya Rais Cooledge. Ndipo wakati "alipoangalia juu," alisema, "Niliona ono la Yesu." Akasema, "Ninaweza kuzungumza lugha tisa mbalimbali, kwa ufasaha." Akasema, "Ila nisingeweza kupata neno moja la kusema, kati ya lugha hizo zote tisa." Akasema, "Kwa hiyo niliinua tu mkono wangu, Naye akanipa mpya, kuizungumza." Akasema, "Ndio kwanza niuone Utukufu wa uso Wake."

37 Mama huyu akaniambia, akasema, "Ndugu Branham, Yesu hakuwa kitu ila mwanadamu, nabii tu."

Nikasema, "Alikuwa Mungu, dada yangu."

38 Akasema, "Unamfanya Mungu, lakini sivyo alivyo." Kwa hiyo akasema, "Akishuka kwenda kwenye kaburi la Lazaro, Biblia ilisema, 'Alilia.'"

39 Hakika, Yeye alikuwa moyo wenyewe wa Mungu. Aliteseka kama sisi tunavyoteseka. Alikuwa mwili kama sisi tulivyo mwili. Alibeba, mwilini Mwake, tamaa zile zile na kadhalika tunazokuwa nazo. Hata hivyo, ili awe Dhabihu kamilifu, ilimbidi kufanya hivyo. Alifanya hivyo. Lakini nilisema . . .

Akasema, "Alilia, akishuka kwenye kaburi la Lazaro."

40 Nikasema, "Lakini, loo, mama, hiyo ni kweli. Yeye alikuwa Mwanadamu, alipokuwa akilia. Lakini aliposimama pale, kando ya kaburi hilo, ambapo mfu mnyamavu alilala; ambapo mwili uliooza ulilala, umefunikwa kwa kitambaa; hapo aliposema, 'Liondoeni hilo jiwe.' Akauvuta mwili Wake mdogo, na kusema, 'Lazaro, njoo huku!' Ndipo mtu aliyekuwa amekufa, siku nne, akasimama kwa miguu yake."

41 Ilikuwa ni nini? Uharibifu ulimjua Muumba wake. Nafsi ilimjua Bwana wake. Naye Mshindi huyo mkuu na mwenye nguvu alithibitisha pale ya kwamba Yeye anazo Nguvu za mauti, na kuzimu, na kaburi.

42 Hakika, inasisimua moyo wetu! Ati mnaongea juu ya kupigapiga masufuria ya kuoshea vyombo, na kupiga honi? Ulimwengu unapaswa kuwa katika yubile asubuhi ya leo, jinsi ambavyo haujawahi kuwa, mayowe na vifijo vya watu Wake, kwa sababu hii ndiyo siku ya ukumbusho ambapo alimshinda adui wa mwisho, na kutuweka huru sisi wafungwa.

43 Naam, Yeye alikuwa Mwanadamu. Hiyo ni kweli. Alithibitisha kuwa Mwanadamu, kisha akathibitisha kuwa Mungu.

44 Usiku mmoja, wakati bahari kuu, inayochafuka, ambayo imechukua maelfu ya maisha . . . Labda baadhi yenu akina mama hapa, asubuhi ya leo, wavulana wenu walikufa kwenye bahari inayochafuka huko nje, wao huenda walizama chini ya mawimbi katika maeneo mapana ya vita vya ulimwengu huu. Baadhi ya wapendwa wenu wamelala huko nje, labda chini ya bahari.

45 Lakini usiku mmoja Yeye alipokuwa amelala katika mashua ndogo, nayo mawimbi yalikuwa yakirukaruka juu ya bahari, kama kizibo cha chupa. Alisimama, akaweka mguu Wake juu ya demani ya hiyo mashua. Akatazama juu Mbinguni, akasema, "Amani." Na kwa mawimbi, akasema, "Tulia!" Nayo bahari hiyo kuu ikatulia hata hapakuwapo na kunyanzi juu yake. Hakika, Yeye alikuwa hivyo!

46 Ni kweli kwamba aliona njaa kama Mwanadamu. Aliposhuka kutoka mlimani Naye alikuwa na njaa, akitafuta kitu cha kula juu ya mti, Yeye alikuwa Mwanadamu. Lakini alipochukua hizo biskuti tano na samaki wachache, na kuwalisha watu elfu tano, Yeye alikuwa zaidi ya Mwanadamu.

47 Alipokufa miaka elfu moja na mia tisa iliyopita, majuzi, akining'inia msalabani, akipiga mayowe apate rehema, "Mungu

Wangu, Mungu Wangu, mbona umeniacha?" Alikufa kama Mwanadamu. Lakini miaka elfu moja mia tisa na kitu iliyopita, asubuhi ya leo, Yeye alithibitisha alichokuwa! Alitoa muhuri wa mwisho wa umasihi Wake alipokatilia kamba za mauti na kuzimu, na kufufuka kutoka kaburini, kwa ushindi, "Mimi ni hai milele! Na, kwa sababu Mimi ni hai, ninyi nanyi mnaishi pia!"

48 Huyo hapo yule Mshindi! Ati unanena kuhusu kunyakua aproni na kuzipeperusha? Watu husema sisi tuna wazimu kwa sababu tunapiga makelele na tunakimbia, na tunapiga mayowe na tunapiga makelele. Hawajawahi kuhisi mitetemo ya ushindi ya Mbinguni, kwamba, "Vita vimekwisha!" Mshindi wetu mkuu, mwenye nguvu ameshinda kila ushindi! Anasimama peke yake, asubuhi ya leo, bila kuguswa!

49 Alipokuja duniani, walimpa jina duni kuliko yote ambalo wangeweza kumpa, kama "mlokole." Wakamwita *Beelzebuli*, "mkuu wa pepo." Hiyo ni kweli. Alienda kwenye mji wa chini kuliko yote duniani, Yeriko, naye mtu mdogo kuliko wote mjini ilimbidi kuangalia chini apate kumwona. Lakini wakati Mungu, miaka elfu moja mia tisa iliyopita, alipomfufua! Hivyo ndivyo mwanadamu alivyomfanyia. Lakini, kwa silaha ya upendo, alimshinda kila ibilisi.

50 Naye Mungu akamwinua juu sana, na kumpa Jina lipitalo kila jina linalotajwa Mbinguni na duniani. Kila jina Mbinguni huliinamia Jina la "Yesu"! Kila Malaika, kila mfalme, kila kitu huliinamia Jina la "Yesu"! Kila ulimi utamkiri, kila goti litamwinamia. Naye amepaa juu sana, hata inambidi kuangalia chini kuziona Mbingu. Huyo ndiye Mshindi mkuu! Huyo Ndiye aliyefanya hivyo! Wakati alipoondoka duniani, baadaye, jana usiku tulikuwa nalo, alikuwa na funguo za mauti na kuzimu zikining'inia ubavuni Mwake, amina, "Msiogope, Mimi Ndimi niliyekuwa nimekufa, na ni hai tena hata milele. Na" (*na* ni kiunganishi) "Ninazo funguo za mauti na kuzimu, zikining'inia papa *hapa*." Nena kuhusu Mshindi! "Na, kwa sababu nilishinda, nilitengeneza tu barabara kuu mpate kuisafiria."

51 Mwanadamu alikataliwa kutoka Mbinguni, barabara kuu zikafungwa. Hakukuwako na barabara kuu. Lakini, ambapo hapakuwa na njia kuu, Yeye alikuja kutengeneza moja. Loo, jamani! Mstari wa kwanza ulikuwa ni pepo wa mashaka, wa pili ulikuwa ubaguzi, uliofuata ulikuwa ubinafsi; dunia hii ilifunikwa na nguvu za mapepo; halafu maradhi, magonjwa. Lakini alipoanza kupaa juu Mbinguni! Jana usiku tulikuwa Naye akitoka kuzimu, akiwa na funguo za mauti na kuzimu ubavuni Mwake. Asubuhi ya leo tunampandisha juu. Haleluya! Alipofufuka, alikuwa na. . . Alipata ushindi. Basi, alipokuwa akipaa juu, alivunja kila nguvu za ibilisi zinazomshikilia mwanadamu. Alipaa Juu, akawapa wanadamu vipawa, vipawa vya Roho Mtakatifu. Yule Mshindi mkuu! Amesimama peke yake, asubuhi ya leo! Na, kati Yake na kila mwaminio, kuna

njia kuu ya zamani ya utakatifu iliyobarikiwa ambayo wenye haki watatembea juu yake. Hakuna njia ya kuepukia. Kuna mstari mmoja tu uliokatwa kutoka Utukufuni. Aliziacha Nyayo zilizojaa Damu alipokuwa akipita kwenye ushoroba wa nguvu za pepo, na kututengenezea njia kuu, kote kote. Yeye ameketi huko Juu, asubuhi ya leo, kama Mshindi mkuu!

52 Watu wake wana yubile. Makumi ya maelfu yao, kote ulimwenguni, wanapiga makelele ya ushindi.

53 Nimekutazama kujiunga huku baridi kwa kawaida kwa kanisa. Naweza kumwazia mtu akisema…Nitakuonyesha kutupwa kwake.

54 Hapa, mara Vita vya Kwanza vilipokwisha, ujumbe ulikuwa ukishuka barabarani hapa, ukaingia kwenye basi la Greyhound. Wakasema, “Kelele hizo zote ni za nini? Zote zinahusu nini?”

55 Ndipo mmoja wao akasema, “Angalia hapa, hili hapa gazeti. Vita vimekoma hivi punde tu.” Na kila mtu analia na kupiga makelele.

56 Lakini mwanamke mmoja alisema, “Loo, jamani, kwa nini ilibidi viishe hivyo?” Kasema, “Kama vingeweza kudumu siku chache zaidi,” kasema, “Mimi na John tungekuwa tukiishi raha mstarehe.” Kasema, “Tungekuwa tumeketi hapo.”

57 Kulikuwako na mtu amesimama nyuma ya mlango wa basi; akamshika mwanamke huyo, na nusura amtupe nje ya mlango. Ndipo polisi walipomkamata mtu huyo, yeye alisema, “Sababu ya mimi kufanya hivyo,” akasema, “mwanamke huyo hakuwa na mtu huko ng’ambo wa kumshughulikia. Lakini nina wavulana wawili huko.” Akasema, “Nisingeweza kuzuilia hisia zangu.”

58 Loo, ndugu! Nina baba huko ng’ambo. Nina wapendwa huko ng’ambo. Ni kitu fulani kwangu, Yesu aliposhinda. Ninaye mke. Nina mtoto mchanga. Nina wapendwa. Yule Mshindi mkuu, mwenye nguvu! Unaweza kuniita “mtakatifu anayejibingirisha” au “shupavu wa dini,” chochote utakacho. Lakini, ninapowazia vile vita vikuu vimetatuliwa, gharama imelipwa, ushindi umepatikana. Yesu alifufuka kutoka kwa wafu, ule muhuri wa mwisho wa umasihi Wake, kwamba yote yamekwisha. Yeye yu hai, asubuhi ya leo, akiwa na funguo za mauti na kuzimu. Nina wapendwa walio ng’ambo ya mpaka huko. Niko kwenye barabara hii kuu ya kale, nikitembea nipate kuwaona. Msifikiri nina wazimu. Loo, lakini nina furaha sana yote yametatuliwa! Ni kazi iliyokamilika.

> Alipoishi, alinipenda; alipokufa, aliniokoa;
> Alipozikwa, aliziondolea mbali dhambi zangu;
> Alipofufuka, alinihesabia haki bure milele:
> Siku moja yuaja—loo, siku tukufu!

59 Ubatizo huu wa kale uliobarikiwa wa Roho Mtakatifu, kutuongoza juu ya hii barabara kuu ya kale ya ajabu sana,

loo, jinsi ilivyo tukufu! Ningewezaje kuuonea aibu? Ninasimama pamoja na Mtakatifu Paulo, asubuhi ya leo, nikisema hivi, “Siionei haya Injili ya Yesu Kristo, kwa maana ni Nguvu za Mungu ziletazo wokovu.” Ni Nguvu juu ya magonjwa. Ni Nguvu juu ya mauti. Ni Nguvu juu ya kaburi.

60 Wakati yule mtume mzee mkali, alipofikia mwisho wa safari yake, nao wakachimba kaburi lake huko nje, nayo mauti yalikuwa yanamkabili usoni, alicheka papo hapo mbele zake. Akasema, “Mauti, u wapi uchungu wako? Kaburi, u wapi ushindi wako?” Ndipo akamsifu Mungu kwa sauti kuu, “Lakini Mungu na ashukuriwe Yeye atupaye ushindi kwa Bwana wetu Yesu Kristo!”

61 Mshindi mwenye nguvu sana aliyepata kuishi, Mshindi mwenye nguvu kuliko wote aliyepata kufa, kwa maana Yeye Ndiye pekee ambaye angeweza kushinda; kufa, na kuyashinda mauti yenyewe, na kufufuka tena kwa ushindi! Alithibitisha kile alichokuwa. Ulikuwa ndio muhuri wa mwisho wa umasihi Wake.

62 Na sasa, kwa bahati, kama kungekuwa na mtu katika jengo hili asubuhi ya leo, ambaye ni mshiriki vuguvugu wa kanisa, wala hajui furaha ya vita kumalizika. Watu hupiga makelele, watu hushangilia, watu hulia! Unasema, “Kwani wana shida gani?” Wanajua ni jambo lililokamilika. Yote yamekwisha! Hakika! Sisi [Ndugu Branham anapiga makofi—Mh.] tunapiga mabendi. Tunapiga kelele kwa baragumu, na Injili inaenezwa. Utukufu na Nguvu za Mungu zinajulikana. Na ni kazi iliyokamilika, mkataba umetiwa sahihi; utukufu kwa Mungu, Kristo aliutia sahihi katika Damu Yake Mwenyewe! Vita vimekwisha. Ushindi umepatikana. Sikuupata; Yeye aliupata! Nina furaha tu juu yake. Jamani!

63 Wakati baadhi ya wavulana hao wakirudi kutoka nchi za ng’ambo, wananiambia, wakati meli ilipoingia New York, ilipokuwa tu ikiingia bandarini, walitazama kule na kuona ile Sanamu ya Uhuru. Ndicho kitu cha kwanza unachoona, kikitokeza. Walisimama, baadhi yao wakiwa ni askari viwete wastaafu huko nje kwenye sitaha ya meli, ili waweze kuiona. Basi walipoanza kuiona hiyo Sanamu ya Uhuru, waliangua kilio. Wakalia. Wasingeweza kujizuia. Mtu mkubwa mno alisimama pale, mtu mkubwa mwenye mikono iliyoparuza, akitetemeka na kutikisika. Wasingeweza kuzuia hisia zao. Kwa nini? Ilikuwa ni nembo ya uhuru. Nyuma tu ya Sanamu hiyo ya Uhuru, walikuwapo...walikuwapo baba, mama, wapendwa, mpenzi, mke, mtoto mchanga, wote katika dunia hii waliowapenda, walikuwa tu nyuma yake. Basi kabla tu hawajaingia, walitambua, ilikuwa ni nchi ya walio huru na makazi ya mashujaa. Hakika, ingetikisa hisia zako, bendera hiyo ya kale ikipepea. Liwazieni, askari mstaafu mwenye makovu ya vita akiingia bandarini! Hakika, ulikuwa ni wakati mzuri sana.

64 Lakini, loo, ndugu, moja ya asubuhi hizi, wakati ile Meli ya kale ya Sayuni itakapopiga king'ora, nami nione nembo ile imesimama pale, ule Msalaba wa kale unaoparuza! Huku pepo zikipeperusha mabango yake ya kijivu, inapopitia kwenye ukungu wa mauti. Ni ushindi ulioje! Mbona, si ajabu hatuwezi kuzituliza hisia zetu! Jambo fulani limetukia; tumekuwa wenyeji pamoja nao. Kitu hicho kimekamilika.

65 Walipolivuka lile daraja kubwa kati ya Australia Kaskazini na—na—na—na Kusini, kutoka Sidney, hadi Sidney Kusini. Jinsi kila mtu alivyochukua. . . Mbona, walienda kote nchini, kujaribu kumtafuta mtu wa kuifanya. Kazi hiyo ilikuwa ni kubwa sana, maana walisema hakuna mtu angeweza kuifanya. Hatimaye, mtu mmoja kutoka Uingereza akasema, "Nitaifanya hiyo kazi." Basi aliposhuka kule kufanya kazi hiyo, alijaribu kila bolti iliyoingia kwenye hilo daraja. Sifa zake zilikuwa hatarini. Alipima matope yote na kila kitu kilichowekwa chini. Akazunguka, na walio bora sana alioweza kuwapata; akachukua makanika walio bora kuliko wote, wanakemia walio bora kuliko wote, walio bora zaidi wa kila kitu alichoweza kupata, karibu naye. Basi, hatimaye, wakati hilo daraja lilipokamilika, na siku ikaja ambapo halina budi kujaribiwa.

66 Wakosoaji wakasimama upande mmoja, wakasema, "Halitastahimili. Litaporomoka. Kuna mchanga mwingi sana huko chini."

67 Lakini alichimba chini, chini, chini, chini kabisa. Alikuwa na imani. Alijua ya kwamba kila kitu kilikuwa kimejaribiwa. Ndipo akasema, "Nitafanya safari ya kwanza kuvuka, mimi mwenyewe." Ndipo alipokuwa akivuka hilo daraja kwa miguu, mbele ya meya, akiwa nyuma namna hiyo; ndipo yale magarimoshi makubwa, kama sita sambamba, yakivuka, yakilitikisa daraja hilo. Mtu mashuhuri aliyelijenga, alitembea mbele ya msafara huu, hivi, "Ikiwa litaporomoka, niko pamoja nalo." Lakini alikuwa na imani.

68 Hivyo ndivyo Bwana wetu mbarikiwa alivyofanya alipolijenga Kanisa Lake! Yeye hupima kila bolti, kila kitu kinachoingia ndani Yake, kwa maana hakina budi kuoshwa kwa Damu! Ndipo mmoja wa wakosoaji aliyekuwa amesimama kando, akasema, "Kundi hilo la watakatifu wanaojibingirisha, hawatafanikiwa." Lakini moja ya siku hizi tukufu! Mshindi huyu mkuu, mwenye nguvu anayetembea mbele yetu leo, mshindi! Acha litetemeke, lifanye litakacho, Yeye ataninii. . . Hakutakuwako na kuteleza hata kumoja ndani yake, popote, kwa maana ameitengeneza njia na kuikamilisha. Hakika!

69 Tunafikiri leo hii juu ya masharti ya watu, kuweka mawazo yetu juu ya mambo ya ulimwengu. Lakini hebu nikwambie jambo fulani, ndugu, kamwe usiniruhusu niionee haya Injili! Loo, ndugu, mimi ni mtu wa mtindo wa kale tu, nimezaliwa

mara ya pili, nimezaliwa na Roho Mtakatifu, kwa Roho wa Mungu. Nilizaliwa hivyo, hivyo ndivyo tu nilivyo, na yote ninayotaka kuwa.

70 Siku moja, si muda mrefu uliopita, kulikuwa na msichana ambaye alikuwa ameenda chuoni. Naye alikuwa maskini msichana mdogo, wa kupendeza. Basi aliporudi nyumbani, alikuja na mawazo yake ya chuoni.

71 Na labda, asubuhi ya leo, baadhi yenu mlikuja na baadhi ya mawazo yenu ya nje. Labda mumeleta, kanisani, mawazo yenu mengi. Naam, yaondoeni, ndilo jambo bora zaidi ninalojua kufanya.

72 Basi msichana huyu, wakati hilo garimoshi liliposimama huko mbele, aliambatana na msichana mdogo, mmoja wa hao maskini vipusa mamboleo, mwajua, kama wa aina ya Elvis Presley. Basi alipokuwa amesimama pale, mwajua, kwenye garimoshi, mama yake alikuwa, huko nje, mwanamke mkongwe aliyesimama pale, amejaa makovu, usoni mwake; maskini mabega yaliyoinama; amevaa maskini nguo ya kaliko, shali ndogo juu ya mabega yake. Naye maskini kipusa huyu mamboleo aliyekuwa pamoja naye, msichana huyu mwingine, alitazama chini, na kusema, "Vema, ni nani maskini yule mzee mwenye sura mbaya, mwenye mashaka?"

73 Vema, unajua, ilimwaibisha huyo msichana sana, akasema, "Sijui mimi," maana alikuwa nadhifu sana, na alikuwa na mawazo mengi sana ya kilimwengu kichwani mwake. Na alikuwa ni mama yake mwenyewe.

74 Aliposhuka kwenye garimoshi, maskini mama huyo mzee alikimbia, kumkumbatia. Akasema, "Loo, mpenzi, Mungu aubariki maskini moyo wako." Naye akageuza mgongo wake akaanza kuondoka, kana kwamba hakumjua. Aliona aibu, kwa sababu mama yake alikuwa na sura mbaya sana.

75 Ndipo ikawa kwamba, kondakta kwenye hiyo garimoshi, aliijua hadithi hiyo. Akaenda pale, na kuweka mikono yake juu ya bega la msichana huyo, akamgeuza mbele ya hadhara hiyo, kasema, "Huna aibu! Huna aibu!" Kasema, "Nimeona wakati ambapo mama yako alikuwa mrembo mara kumi kuliko wewe ulivyo." Kasema, "Alikuwa . . . Niliishi katika ujirani." Kisha akasema, "Ulikuwa mtoto mchanga, na ulikuwa ghorofani kwenye kitanda chako kidogo. Naye mama yako alikuwa akianika nguo kwenye kitalu cha nyuma." Kisha akasema, "Mara ghafla, tanuru ilishika moto, na nyumba nzima ikaanza kuteketea. Ndipo maskini mama yako alipokimbia, na akijua ya kwamba ulikuwa ghorofani, kule juu." Kasema, "Walipiga mayowe, na kujaribu kumshika kwa nguvu. Lakini yeye akavuta alichokuwa nacho, akakiacha, na kukimbia kupitia kwenye ndimi hizo za moto, juu kwenye vipandio; kisha akatoa nguo zake mwilini mwake, na kukufunika nazo. Naye huyu

hapa anakuja, akirudi kupitia kwenye ndimi hizo za moto, amekubeba. Naye akazimia, barazani, na huku amekushika mikononi mwake." Kisha akasema, "Alichukua kile ambacho kingemkinga, akakukinga wewe." Kisha akasema, "Sababu ya wewe kuwa mrembo leo hii, hiyo ndiyo sababu yeye ana sura mbaya. Basi, unataka kuniambia, ungeyaonea aibu makovu hayo ya mama yako?"

Nafikiri leo hii:

> Ati Yesu aubebe msalaba peke yake,
> Na ulimwengu wote uwe huru?
> Kuna msalaba kwa kila mtu,
> Na kuna msalaba kwa ajili yangu.

76 Ikiwa Yesu alihesabiwa kuwa "Beelzebuli," na ulimwengu huu, alichekwa na kudhihakiwa, na kutundikwa msalabani, akafanywa aibu kwa ajili yangu, nina furaha hata na zaidi kubeba lawama ya utakatifu Wake. Ndiyo, bwana. Niite, "Mtakatifu anayejibingirisha!" chochote unachotaka kuniita, matamshi yote unayotaka kutoa. Hiyo hailizuii hata kidogo. Nina furaha tu, asubuhi ya leo, kwamba, moyoni mwangu, Kristo aliyefufuka anaishi na kutawala. Mimi ni mmoja wa raia Wake. Natumaini kwamba ndivyo ulivyo, pia.

77 Muda wetu umeenda sasa. Ni saa moja kamili, tuliposema tutafumukana. Ibada zijazo zitaanza baada ya kama saa mbili, sasa, saa tatu na nusu.

Hebu na tuinamishe vichwa vyetu, kwa muda mfupi tu, katika maombi.

78 Baba wa Mbinguni mbarikiwa, dakika arobaini na tano zimepita, Neno limetolewa. Mioyo yetu ina furaha. Yubile inaendelea; sio tu yubile ya siku moja, bali yubile ya Milele! Utukufuni, Malaika wanaimba. Ee Mungu, Kanisa, lililoshinda, linaimba. Kengele za furaha zinalia. Nafsi ambazo wakati mmoja zilihukumiwa kifo, na kufa na kwenda kwenye kaburi la ibilisi; huyo ibilisi ameshindwa! Mauti yameshindwa. Kaburi limeshindwa. Magonjwa yameshindwa. Ushirikina umeshindwa. Kijicho kimeshindwa. Chuki imeshindwa. Kutokujali kumeshindwa. Ugumu umeshindwa. Ubinafsi umeshindwa. Kila kitu kimeshindwa. Kristo ndiye Mshindi mkuu!

> Lo! mtazameni Mshindi Mwenye nguvu, (alisema mshairi)
> Lo! mtazameni amewekwa wazi,
> Kwani Yeye ndiye Mshindi Mwenye nguvu,
> Tangu alipolipasua lile pazia vipande viwili.

79 Alilipasua lile pazia lililomficha mwanadamu kutoka kwa Mungu, na sasa Mungu anaishi miongoni mwa wanadamu. Alilipasua pazia lile lililouzuia uponyaji wa Mungu. Alilipasua lile pazia lililozizuia baraka za Mungu. Alilipasua lile pazia

lililoizuia furaha ya Mungu. Alilipasua lile pazia lililoizuia amani ya Mungu. Sasa pazia limepasuliwa vipande viwili. Kwa Damu Yake Mwenyewe, alitembea kama Mshindi! Vita vimekwisha, alituthibitishia katika ufufuo Wake. Na sasa Roho Mtakatifu ni shahidi, ametumwa kutuongoza.

80 Ee Mungu wa Milele, kukiwako na mtu hapa asubuhi ya leo, ambaye amechezacheza tu njiani, kuingia na kutoka, kutoka kwenye barabara kuu, akianguka kando ya njia; hajawahi kutembea moja kwa moja katikati, pamoja na wale mashujaa wakuu, wale mashujaa wakuu ambao wamekanyaga katikati ya barabara kuu; tunaomba, asubuhi ya leo, kwamba watatoa yote yao Kwako, na kutoka na kufurahia ushindi huu mkuu ambao Bwana wetu aliyefufuka ameupata. Tujalie, Baba, kwa kuwa tunaomba katika Jina la Kristo.

81 Na huku tukiwa tumeinamisha vichwa vyetu. Nashangaa, katika muda huu wa wakati, ya kwamba kama ungemwinulia Kristo mikono yako, na kusema, "Kristo, ninashukuru, sitakuonea aibu tena. Nimekuwa tu mwoga kidogo." Mungu akubariki, mama. Mungu akubariki, bwana. Mungu akubariki, wewe. Loo, jamani, mikono ikienda kila mahali! "Kidogo nimekuwa mwoga. Kidogo nimeona aibu. Na kweli naona mahali pangu sasa. Sikupaswa kufanya hivyo kamwe. Ninapaswa kusimama moja kwa moja, kutoa ushuhuda wangu! Ninapaswa kuwa hivyo hasa. Ninapaswa kumwambia kila mtu, 'Nimezaliwa mara ya pili.' Ninapaswa kumwambia kila mtu, 'Nimempokea Roho Mtakatifu.' Siionei haya Injili, kwa maana ni Uweza wa Mungu uletao wokovu. Ninataka kuwa Mkristo halisi wa mbele. Sijawa. Lakini, kwa msaada wa Mungu, tangu asubuhi hii ya Pasaka, nitakuwa. Nitakuwa." Mtu mwingine utakayeinua mikono yako sasa kabla hatujaomba? Mungu akubariki, wewe, wewe.

82 Jamani, angalia maamuzi! Angalau ishirini na tano au thelathini, wanaoketi miongoni mwa kundi hili dogo la watu asubuhi ya leo, wamefanya uamuzi. Kutoka asubuhi hii kuu ya ushindi, wanaenda, kwa neema ya Mungu, kujitokeza na si kuionea haya Injili, kwa kuwa ni Nguvu za Mungu ziletazo wokovu.

83 Ee Mungu, wakati mikono hii inapoinuliwa, nao muziki unarudisha mwangwi kwa utamu barabarani, kwa kuwa tumepita kutoka mautini kuingia Uzimani, kwa kuwa Wewe umesema, "Yeye ayasikiaye Maneno Yangu, na kumwamini Yeye aliyenipeleka, yuna Uzima wa milele." Wamepita kutoka mautini kuingia Uzimani, kwa sababu Wewe ulifanyika mauti wapate kuwa Uzima, kupitia kufufuka Kwako. Ulifanywa mdogo punde kuliko Malaika, ukashuka uwe mwanadamu, ukatoka kwenye hiyo Thiofania kuu kutoka huko Ng'ambo, aliyefanyika mwili na akawa na Damu, kisha akaimwaga hiyo Damu, ili Wewe upate kufanya njia ya kuepukia kwa

ajili yetu sote. Basi si kwamba tu ulifanya hivyo, (tunalisoma katika Biblia), bali ulilithibitisha, bila kukosea, kwa kufufuka kutoka kwa wafu, na kuwafufua wafu ulipokuwa hapa duniani; si hivyo tu, bali Wewe umetoa, umelifanya thibitisho maradufu, kama ulivyomfanyia Ibrahimu; sasa, pamoja na hayo, ulimrudisha Roho Mtakatifu kama shahidi. Nasi tuna Uwepo Wake uliobarikiwa pamoja nasi, na ndani yetu, ukituongoza, ukituongoza katika Kweli yote na Nuru.

84 Tunakushukuru Wewe kwa mikono hii mingi ambayo imeinuliwa, asubuhi ya leo, ikisema, "Sasa ninamchukua Kristo kama wangu." Ee Mungu, kama hawajawahi kubatizwa majini, kuwakilisha mauti kuu, kuzikwa, na kufufuka kwa Bwana wao mbarikiwa, jalia warudi kwenye ibada asubuhi ya leo, wakileta nguo zao, na tayari kushuka kwenye dimbwi hili baridi sana. Tujalie, Baba.

85 Utubariki. Utusamehe dhambi zetu. Tutakupa Wewe sifa, katika nyakati zijazo. Wakati vita vimekwisha kabisa, wakati moshi umekauka kabisa, na furaha imekamilika kabisa, ya midomo hii ya duniani, ambapo tunakusifu Wewe kwa kila kitu tulicho nacho, itabidi tuwe na sauti mpya, viumbe vipya, kukusifu Wewe kwavyo. Na tuingie basi kwa furaha. Kwa kuwa tunaomba katika Jina la Kristo. Amina!

86 Hebu na tusimame kwa miguu yetu sasa...?...Msisahau zile ibada, saa tatu na nusu. Nendeni nyumbani, mpate kifungua kinywa chenu. Rudini, tunatarajia kuwa pamoja nanyi sasa. Na kisha usiku wa leo, kumbukeni. Sina budi kuondoka alasiri ya leo, na kusoma na kuomba.

87 Kwa kuwa nawaambieni, ya kwamba, Kristo yu hai, Yeye hajafa. Nami naamini, kwa moyo wangu wote, Yeye atakuwa moja kwa moja katika jengo hili usiku wa leo, kuonyesha ya kwamba Yu hai, kufanya mambo yale yale ambayo Yeye alifanya katika asubuhi ile ya kwanza ya Pasaka na katika safari Yake ya maisha. Kama sivyo, basi nimekuwa nabii wa uwongo. Nina furaha sana kujua ya kwamba katika saa hii kuu ya giza tunayoishi sasa, wakati matumaini yote, inavyoonekana, yametoweka; Kristo, ule Mwamba imara tunaweza kusimamia, misingi mingine yote ni mchanga udidimiao. Vema.

88 Wimbo wetu mdogo, wa kufumukana, wa *Peleka Jina La Yesu*. Kila mmoja, pamoja sasa.

> Peleka Jina la Yesu,
> Mtoto wa huzuni na majonzi;
> Litakupa furaha na...

89 Geuka moja kwa moja, na kupeana mikono, na kusema, "Bwana asifiwe," kwa mtu aliye karibu nawe. (Vema, Bwana asifiwe...?...)

Tumaini la duniani na furaha ya Mbinguni;
Jina la thamani, Loo ni tamu jinsi gani!
Tumaini la duniani na furaha ya Mbinguni.

90 Sasa kila mtu aangalie moja kwa moja huku? Tumsifu tu. Hebu inua tu mikono yako, na useme, "Asante, Bwana, kwa kuokoa nafsi yangu." Vema, kila mtu!

Asante, Bwana, kwa kuokoa nafsi yangu.
Asante, Bwana, kwa kunifanya mzima.
Asante, Bwana, kwa kunipa,
Wokovu Wako mkuu uliojaa sana na bure.

91 Ni jambo lenye baraka jinsi gani! Mnampenda? Semeni, "Amina." Loo, ninii. . . Kila kitu kimekamilika sasa, watoto. Kila kitu kimekwisha, hakuna vita tena, hakuna vita tena, hakuna unachopaswa kufanya; tayari kimefanywa. Tunashangilia tu! Loo, jamani! Tumekamilika, ndani Yake!

. . . ninaegemea,
Salama salimini kutoka kwenye hatari zote;
Ninaegemea, ninaegemea,
Ninaegemea kwenye mikono ya milele.

Loo, ni tamu jinsi gani kutembea katika njia hii ya msafiri,
Nikiegemea kwenye ule Mkono wa milele;
Loo, jinsi njia inavyozidi kuwa angavu siku baada ya siku,
Nikiegemea kwenye mikono ya milele.

Kuegemea, kuegemea,
Salama salimini kutoka kwenye hatari zote;
Ninaegemea, ninaegemea,
Ninaegemea kwenye mikono ya milele.

Ninyi mnaoweza, na mlio na leso, zitoeni.

. . . loo, kuegemea,
Salama salimimi kutoka kwa hatari zote;
Ninaegemea, ninaegemea,
Naegemea kwenye mikono ya milele.

Sasa Biblia yako!

Ninaegemea, ninaegemea,
Salama salimini kutoka kwa hatari zote;
Ninaegemea, ninaegemea,
Ninaegemea kwenye mikono ya milele.

92 Ni nini? Salama na kulindwa, kote, yote yamekamilika, vita vimekwisha, muhuri wa mwisho umevunjwa, Yeye amepaa juu. Haleluya!

Ninaegemea, ninaegemea,
Salama salimini kutoka kwa hatari zote;
Ninaegemea, ninaegemea,
Ninaegemea kwenye mikono ya milele.

93 Sasa na tuinamishe vichwa vyetu kuelekea mavumbini ambapo Mungu alituchukua, ambapo siku moja tutapanda kutoka katika mavumbi ya nchi. Kwa maana, Bwana wetu, aliyeletwa kutoka mavumbini, akaingia mavumbini, ili kutupa Roho Wake asiyepatikana na mauti, alipaa juu kutoka mavumbini, na wale wote walio ndani Yake, watapaa pamoja na Yeye siku moja, kwenye maeneo ya waliobarikiwa.

94 Tunapoinamisha vichwa vyetu, naona Ndugu Smith yuko katikati yetu, asubuhi ya leo, mchungaji wa Church of God; alinipigia simu jana usiku. Ndugu Smith, naomba ushuke moja kwa moja. Nashangaa sasa, kama Ndugu Smith atatufumukanisha kwa maombi mafupi. Mnapoharakisha kwenda nyumbani kwenu, mpate kifungua kinywa chenu. Mrudi kwenye ibada ya Shule ya Jumapili, na ibada ya ubatizo, mara kuanzia saa tatu na nusu. Na tuinamishe vichwa vyetu, wakati Ndugu Smith anapoturuhusu tuondoke kwa maombi.

Mshindi Mkuu Na Mwenye Nguvu SWA57-0421s
(The Great And Mighty Conqueror)

Ujumbe huu uliohubiriwa na Ndugu William Marrion Branham, uliotolewa hapo awali katika Kiingereza mnamo Jumapili ya Pasaka asubuhi kwenye mapambazuko, tarehe 21 Aprili, 1957, katika Maskani ya Branham huko Jeffersonville, Indiana, Marekani, umetolewa kwenye kanda ya sumaku iliyorekodiwa na kuchapishwa bila kufupishwa katika Kiingereza. Tafsiri hii ya Kiswahili ilichapishwa na kusambazwa na Voice Of God Recordings.

SWAHILI

©2022 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org

Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

Voice Of God Recordings
P.O. Box 950, Jeffersonville, Indiana 47131 U.S.A.
www.branham.org